

Pepo: Makazi ya kudumu ya WachaMungu

Harun Yahya

**Mfasiri
Box 90399
Dar es Salaam**

Neno la Mfasiri

Kuandaliwa kwa Kitabu hiki ni jitihada ya kujaribu kutoa picha halisi na muelekeo sahihi unaofunzwa na Uislamu kinadharia juu ya maisha ya Peponi. Pepo ni umbile tukufu ambalo ni zawadi watakayotunukiwa watu na majini watakaofuzu mtihani wa maisha ya ulimwenguni kwa matendo yao mema kulingana na alivyoamrisha Muumba. Kitabu hiki kinatoa picha ya jumla na ya kweli juu ya umbile la Pepo na maisha ya Peponi ili kuwaongezea tamaa na hamu wale wote wanaofanya jitihada ya kumcha Mwenyezi Mungu. Hamu na tamaa ambazo kwa Tawfiq ya Mwenyezi Mungu zitawapa hamasa ya kuzidisha na kudumisha matendo mema, yatakayowafanya wafanikiwe na wawe mionganoni mwa wakazi wa umbile la Pepo lenye jiografia ya ajabu. Maudhui ya kitabu hiki yanamjenga msomaji aweze kukabiliana na changamoto za kuepuka makatazo na kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa matarajio ya kufaulu na kuingia Peponi.

Dhana na picha ya kimawazo inayochorwa na kitabu hiki, ni nyenzo za kumsaidia msomaji kupata taswira na kuuchambua ukweli juu ya maisha haya. Inatarajiwa nyenzo hizo ziwe msukumo wa kufanya utafiti wa kina ili kupata usahihi juu ya dhana, itikadi na maelezo mengi yatolewayo juu ya maisha yajayo yenye uhai wa milele. Usaидizi wa nyenzo hizo, utamuwezesha msomaji kubaini hakika juu ya maisha ya Peponi na kuweza kuyasawiri kifikra akiwa na hakika nayo.

Kwa kuwa ufahamu juu ya maisha ya Peponi umezungukwa na hakika za kiimani, basi ulinganishi uliofanyika kitabuni humu unawianishwa na maisha halisi ya ulimwengu huu. Katika baadhi ya sura au sehemu, yametolewa maelezo linganishi ili kumuwezesha msomaji kupima na kutafakari ili kupata uoni huru unaotokana na hakika za kimsingi zenye hoja madhubuti. Kitabu hiki kimelenga kusaidia kumpa msomaji uhalsia wa kile ambacho pengine amekuwa akikisikia, kujifunza na kukiamini muda wote bila ya kuwa na walau tawira yake.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aikubali jitihada hii, atusamehe upungufu wetu na atie Tawfiiq wasomaji wake waweze kuyafahamu vyema maudhui ya kitabu hiki na ili kwayo, waweze kuishi kulingana na atakavyo YEYE, wapate kufaulu na kuzawadiwa Pepo tukufu katika maisha yajayo ya Akhera baada ya haya ya Ulimwengu.

Sura ya Kwanza

Pepo ni Nini na Kupi Kufanikiwa kwa Kweli

Qur'an, ufunuo kutoka Mwenyezi Mungu Muumba wa kila kitu, inaieleza Pepo kwa lugha ya picha yenye umbile lenye mandhari, mazingira na hali ya kijiografia inayotofautiana na maumbile ya Ulimwengu huu. Pepo ni moja ya maumbile yanayounda mandhari ya Akhera. Akhera kama ulivyo Ulimwengu, ni ombwe linalokusanya maumbile anayoyajua Mwenyewe Mwenyezi Mungu, moja wapo likiwa Pepo yake tukufu. Peponi si mbinguni wala Pepo si mbingu, bali ni umbile ambamo ndimo yalimo makazi matukufu yaliyoandaliwa rasmi kwa ajili ya majini na watu walioishi kwa kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu hapa Ulimwenguni.

Ilivyokuwa Dunia ni makazi ya muda ya Watu, majini, wanyama, wadudu na viumbwa vyenginevyo, iliyowekewa kila kilichohitajika katika kuwezesha maisha yao yakiwemo maji, hewa munasibu, vyakula na kila kilichohitajika, Pepo kwa upande wake imeandaliwa kuwa makazi ya waja wema tu ikiwa imewekwa vyakula, matunda, vinywaji visivyoondoa akili, burudani zisizo za kipuuzi, nguo na hewa ya aina yake, majengo, mito, mabwawa, mabustani yaliyopangwa vizuri, vijja, njia na barabara zilizojengwa tayari kwa ajili ya matumizi ya wakazi wake watarajiwa. Tofauti na ilivyokutwa dunia zama za awali za maisha ya watu, ikiwa haina majengo bali misitu, wanyama, wadudu, mito, mabwawa, bahari na majangwa; mpango wa ujenzi wa Pepo umefanywa na Mwenyewe Mwenyezi Mungu, kwa hiyo atakaefuzu na kupata zawadi hiyo atakuwa amefaulu kwa kiwango kisichoweza kumithilishwa.

Hata hivyo, mawazo yaliyomea na kustawi duniani kote hivi sasa ni kwamba, maisha ya mtu yatakuwa yamekamilika baada ya yeye kupata utajiri au kuwa na mume au mke mwenye heshima na hadhi za kidunia katika jamii kwa sababu ya cheo au nafasi yake nzuri. Qur'an haiyakubali mawazo haya kwani yenyewe inasema kuwa maisha haya ya dunia kamwe hayatifikia mahala pa kukamilika na kutokuwa na changamoto au matatizo kwani maisha yenyewe yamekusudiwa kuwa mtihani.

Mzizi wa neno "dunia" una maana pana sana. Ni kiyambishi cha kisifa "daniy" chenye maana ya duni, isiyo na raha, yaani chini na isiyo na maana kabisa. Kwa hiyo Dunia maana yake ni mahali penye sifa hizo. Ndiyo maana Qur'an, mara zote inayaponda maisha ya dunia kuwa si chochote na hayana maana yoyote. Inavitaja vitu kama utajiri, mali, mume, mke au wake, watoto, hadhi na mafanikiyo ambayo ndiyo yanayodhaniwa kuwa yanayafanya maisha yawe mazuri kuwa si chochote na ni ya kupita tu na ya hadaa.

Katika aya moja ya Qur'an Mwenyezi Mungu anasema:

Juweni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi na pambo na kufurahishana baina yenu(kwa nasaba), na kufurahishana kwa mali na watoto.(Na hali ya kuwa vyote hivi hamdumu navyo. Mfano wake) ni kama mvua ambayo huwafurahisha(wakulima) mazao yake kisha yanakauka, ukayaona yamepiga umanjano kisha yanakuwa mabuwa(hayana chochote). Na Akhera kuna adhabu kali(kwa wabaya) na piya msamaha wa Mwenyezi Mungu na radhi yake(kwa wema). Na hayakuwa maisha ya dunia ila ni starehe idanganyayo(mara huondoka).(57:20).

Aya nyingine inayoelezea jinsi watu wanavyopofushwa na maisha bandia ya dunia ni hii;

“Lakini nyinyi mnapenda zaidi maisha ya dunia. Hali ya kua maisha ya Akhera ndiyo bora(zaidi kabisa) na yenyenye kudumu(87:16-17).

Kama isemavyo aya hiyo, watu hawa huyachukulia maisha haya ya dunia kuwa ni bora kuliko yale ya Akhera na kwamba ndio mwisho wa kila kitu na hakuna maisha mengine. Mtazamo huo dhaifu huwafanya wakane imani juu ya Allah na Kitabu chake.

Allah anawaelezea watu hawa kama:

“Wale wasioogopa kukutana na sisi na wakawa radhi na maisha ya dunia na wakatuwa kwayo, na wale walioghafilika na aya zetu(10:7).

Na Qur'an inabainisha kuwa watu hao watakutana na mateso ya kudumu Jahannamu. Hata hivyo upungufu hauna maana kuwa dunia haina vitu vizuri la hasha! Allah ameujazia ulimwengu vitu vizuri vyatika kutukumbusha Pepo. Mazuri ya Peponi na mabaya ya motoni yakiwa yametahafifishwa yamechanganywa pamoja hapa duniani kwani hapa duniani ni pahala pa mtihani. Kwa hiyo wale walioamini hupata hisia za starehe zote mbili na hivyo basi badala ya kukumbatia maisha haya mafupi ya muda, wao huyaelekeea yale maisha halisi ya milele.

Qur'an inailezea Akhera kuwa ndiyo makazi halisi na ya milele ya kila mtu. Lakini pamoja na ukweli huo watu wengi hudhani wanaweza kujitengezea maisha kamili hapa hapa duniani. Wanautazama upungufu kama wa maradhi, uchovu, maumivu, hofu, wasi wasi na mashaka kuwa ni mambo ya kawaida ya kimaumbile. Lakini kumbe Allah ameumba upungufu huu kwa makusudio yaliyofichikana, ili watu wayatafakari barabara makusudio hayo na wapate mafundisho sahihi. Ni jambo ambalo lingwezekana kabisa kwetu kuishi bila ya kuuguwa, kusikiya uchovu unaotulazimu kupumzika na kulala. Watu wangeliweza kuwa na stamina na nguvu za kuishi bila kuchoka kama Mwenyezi

Mungu angalitaka tuwe hivyo. Angeweza kutuumba bila ya upungufu au matatizo hayo lakini hasha, yeye ametuumba na upungufu na matatizo hayo ili tujielewe kuwa, sisi ni viumbe dhaifu tusiojitegemea wenyewe.

Kila mtu hulazimika kukabiliana na udhaifu na unyonge wake katika maisha yake. Ila wakati kiwiliwili chake ambacho mwenyewe anakiona bora sana daima humkumbusha udhaifu wake. Aamkapo kila asubuhi na kuianza siku, uso wake huwa umevimbiana na huwa ovyo ovyo. Kinywa chake huwa harufu mbaya na yej huwa anajisikia ovyo kwa sababu ya uchafu katika ngozi, nywele na mwili mzima.

Iwapo haogi sawa sawa basi hawezi kuondokana na hali hii ya kujisikia ovyo ovyo. Tena basi, kuoga huko lazima kurudiwe mara kadhaa kwa siku kwani kila baada ya kupita muda fulani uchafu hurudi tena mwilini. Na akipitisha siku chache tu bila kuoga, lazima ya kuoga huongezeka na hudhihirika kwani hufikia mahala pa kuwafanya wenzie waliokaribu naye wakose raha kabisa. Mwili wa binaadamu siyo mgumu kama jiwe au metali bali wenyewe umejengwa na vitu vinavyoharibika haraka zaidi, vitu hivyo ni pamoja na nyama.

Mwili huu unafunikwa na ngozi nyembamba inayoweza kuchanika wakati wowote inapopata ajali ndogo tu. Kwa jumla nyama ya kiwiwili ni rahisi sana kuathirika. Yaweza kujeruhija, kuchubuka na kukunjamana kwa kipigo kidogo kabisa. Na kadri umri unavyokwisha mtu huanza kupoteza unyororo, unga'vu na husinyaa, kukauka na kukunjamana. Baada ya kufa, huanza kuoza. Majuma machache tu baada ya kuzikwa mwili huanza kuchakachika, kuliwa na mabubu na hatimaye huchanganyikana na udongo na kutoweka kabisa.

Upungufu wa kimaumbile alionao Mwanaadamu umeumbwa kwa makusudi maalumu. Udhaifu huwo unatukumbusha kwamba tupo duniani kwa makusudio maalumu. Chanzo cha umbile la Mwanaadamu ni udongo na baadaye

nyama. Badala ya nyama wangaliweza kuumbwa kwa vitu vingine bora zaidi au wangeweza kuumbwa katika hali ya kutosikia maumivu, kutopata magonjwa na kutokudhurika. Lakini hasha, yote hayo yameumbwa kwa minajili ya kuwakumbusha Wanaadamu jinsi walivyo dhaifu na jinsi wanavyohitaji msaada wa Allah licha ya hiyari, utambuzi na uhuru waliotunukiwa katika kuendesha maisha yao. Sifa kuu ya Mwanaadamu juu ya viumbwa vyengine ni kwamba, yeche si mtambuzi tu bali ni mtambuzi wa nafsi yake. Si hivyo tu bali upungufu walionao, unawaonesha kuwa makazi ya hapa duniani si ya kudumu na yeche si mtawala wa mwisho wa mambo yake. Tunapouangaliya upungufu huu twaweza kujiona udhaifu wetu na kuielewa starehe ya mpito ya madaraka na mazuri yote ya dunia hii. Wakati huo huo huwalewa watu wanaoabudiwa badala ya Muumba, tunaajaribu kuwfurahisha au kuwatukuza. Kumbe na wao ni dhaifu, wana upungufu kama watu wengine. Lakini wengi hawalewi hili na hawaoni udhaifu na upungufu wa dunia, ndiyo maana wanahangaika na starehe za maisha ya dunia hii. Kwa hakika haya ni matokeo ya ujinga na matokeo ya kushindwa kukitumia vyema kipawa cha akili tulichotunukiwa. Mwenendo huo unaelezwa hivi katika Qur'an:

“Basi jiepushe na wale waupao kisogo ukumbusho wetu huu(Qur'an). Na wala hawataki ila maisha(ya starehe) ya dunia. Hakika Mola wako ndiye amjuaye anayepotea njia yake, na ndiye Amjuaye anayeongoka(53:29-30).

Wale wasioujua ukweli huu ndio wanaoshikwa na matamanio ya maisha haya ya dunia. Hao ni watu wasioelewa kitu kama aya isemavyo. Sasa basi ni ufahamu gani tunaotakiwa kuwa nao katika jambo hili? Kwa kweli si kingine bali ni elimu ya Pepo ambayo Allah ametuhadi. Hatuwa muhimu kabisa ya kuiendea Pepo hiyo ni kuielewa vema Qur'an na kutafakari kwa makini yale inayoyasema. Katika Qur'an Mwenyezi Mungu anayaelezea makazi halisi ya waumini kwa maneno haya:

“Na hayakuwa maisha ya Dunia ila upuuzi na mchezo; na nyumba ya akhera ndio maisha hasa: Laiti wangalijua(29:64).

Hadithi inamkariri Mtume(s.a.w) akisema kuwa pepo ni makazi halisi ya Wanadamu, ni mahali ambapo hapatakuwa na udhaifu wa kibinaadamu. Mwenye kunadi atanadi, mtakuwa na ubukheri wa afya wa milele, katu hamtaugua, mtakuwa na uhai wa milele, katu hamtakufa, mtakuwa na ujana wa milele katu hamtazeeka, na raha ya milele, katu hamtakuwa katika hali ya kutotosheka(Muslim). Qur'an inawaahidi Waumini kufaidi kukubwa na malipo yasiyokoma, na starehe za milele za maisha ya Peponi.

Kwa vile waumini wameahidiwa Pepo basi hata hapa duniani wataneemeshwa kwa rehma na ukarimu mkubwa wa Allah(s.w). Qur'an inasema kuwa Waumini wanaotenda mema katika Dunia hii pia watapewa maisha mema hapa Duniani.

“Wafanyaji mema, wanaume au wanawake hali ya kuwa ni Waislamu tutawahuisha maisha mema na tutawapa ujira(Akhera) mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokuwa wakiyatenda(16:97).

Katika aya nyinginezo ahadi hiyo njema inasema wataifaidi waumini wote wa kweli, Mitume ndiyo wakiwa wa mwanzo mionganini mwa waumini. Kwa mfano Mtume Muhammad(s.a.w) ambaye katika Qur'an amepewa habari njema za vyeo vyaya juu peponi, alikuwa ni mtu ambaye Allah alimtajirisha hapa duniani.

“Na akakukuta fakiri akakutajirisha(93:8).

Mbali ya hivyo, Qur'an pia inatutajia utajiri wa mali walizopewa Manabii Daud, Suleiman(a.s), Ibrahim(a.s) na watu wema kama Dhul Qarnain. Kutowa neema na starehe dunia hii kama ujira na motisha na kama ishara ya Rehema na

Mapenzi ya Allah kwa waumini wa kweli ni moja kati ya kanuni za kudumu za Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa utajiri, raha na sterehe ndizo sifa kuu za Peponi, Mwenyezi Mungu kaumba mfano wa neema hizo hapa duniani, kama ukumbusho kwa wale aliowichagua kuingia Peponi. Na ili kuwaongeza hamu na uchu wa kupata Pepo. Swala wanazoswali na kila jema wanadolifanya, liwe kubwa au dogo ili kupata radhi zake. Mbali na yote hayo, wao pia hujua kuwa Malaika huziandika amali zao katika madaftari na kwamba watalipwa Akhera kwa yale waliyoyafanya. Hii ni hisia ya kujichunga ambayo inatokana na kule kuelewa kwao kuwa Allah amewasaidia kwa Majeshi ya Malaika mbele yao na nyuma yao ili wawalinde kwa amri ya Mwenyezi Mungu:

“Ana(kila mtu) kundi la Malaika mbele yake na nyuma yake. wanaomfutilia kwa amri ya Mwenyezi Mungu.(13:11).

Kwa hali hiyo watazishinda nguvu zote za upinzani wanazokabiliana nazo katika njia ya Mwenyezi Mungu na daima wao huwa na shauku ya ile ahadi nono ya Pepo. Hivyo waumini wa kweli kama Allah alivyowaambia Malaika hawatokuwa na hofu wala unyonge kwani:

(Kumbukeni) Mola wenu alipowafunulia Malaika(akawaambia): Hakika mimi ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu wale walioamini nitatia woga katika nyoyo za makafiri, basi wapigeni katika shingo(zao) na kateni kila ncha za vidole vyao.(8:12).

Sura ya Pili

Kutamani Maisha ya Raha

Ni kipi hasa Mwanaadamu anachokistaajabu, anachokihusudu, anachokitaka, anachokihitaji, anachokitamani au kukipenda zaidi katika maisha? Nyumba nzuri, jumba kubwa la fahari, mavazi ya gharama kubwa, mapesa, utajiri au mali na jaha? Ni hisia zipi ambazo mtu huzipata anaposimuliwa habari inayohusu mahali fulani ambako kila kizuri atakacho na akipendacho ataweza kukipata tena kwa kudumu nacho milele? Bila shaka anafurahi sana na atapenda kufika mahali hapo tena ikiwezekana sasa hivi. Yumkini hakuna mtu ambaye aweza kufanya ajizi au kukataa kwenda kuishi mahali pazuri pa namna hiyo.

Hebu sasa fikiria jambo hili: Je kuna mtu yejote ambaye amewahi kusimulia habari kuhusu pale mahali penye neema nyingi au palipo jaa neema zisizo na hesabu. Pale ambapo kila kizuri, kila kitamu, kila kinono, kila kipendacho roho kitasogezwa miguuni mwake?

Bila shaka si mara moja wala mbili na si mtu mmoja wala si wawili, lazima watakuwa wamewasimulia wengine kuhusu kuwepo kwa maisha fulani, nayo ni maisha ya peponi ambako kila anachokihitajia mtu kimekwisha andaliwa kwa ajili yake.

Kila mtu ana khabari kwamba baada ya mauti kuna maisha haya ya milele ya peponi. Wale watakaostahiki kuingia humo watakuta kila kitu wanachokitamani. Watapata malipo yao ambayo ni ya kuishi mahala pema penye neema na starehe za kudumu. Waumini watakaofuzu majoribio au watakaofaulu mtihani wa maisha haya ya dunia, hao Mwenyezi Mungu amewaahidi makazi mapya na ya kipekee. Muda mfupi wa saa, moja, siku moja au miaka mia

anayoishi mtu hapa duniani kwa upande wake, ni fursa ndogo tu ya kutafutia makazi hayo mazuri.

Sasa nini basi kinachowakosesha watu hamasa ya khabari hii njema ya pepo? Ni nini kinachowazuia wasitamani Pepo, nini kinachowatia uzito kufanya jitihada za kuipata? Kwa nini watu, licha ya kujua kuwa watapata neema za milele kama malipo ya Mola wao lakini bado hawajiandai kwa ajili ya neema hizo?

Kwa hakika sababu kubwa kabisa ni kwamba baadhi ya watu hawana yakini kuwa pepo ipo: Wengine hawaamini kabisa, wengine wameifanya ni kitu cha kufikirika na wengine wamekuwa wakiihusisha na mambo ya kiroho kwa ile tafsiri potofu ya roho. Zinaweza kuwepo sababu nyingine za watu kutoamini au kuitilia mashaka Pepo. Jambo la msingi ambalo sote hatuna budi kulitilia maanani ni kuwa mashaka haya wakati mwingine yanatokana na uhaba, uchache au ukosefu wetu wa elimu na pengine mtindo au njia zinazotumika katika kuelezea uyakini na uhalisia wa maisha yajayo.

Mazingira ya Peponi

Kwa hakika si dhambi Waislamu kuishi maisha ya starehe na ya kitajiri hapa duniani muda wa kuwa wanazingatia mipaka ya Allah na wanamcha ipasavyo, kwani rasilimali za dunia(nguo nzuri, chakula kinono, majumba mazuri) zimeumbwa kwa ajili ya waja wa Mwenyezi Mungu kama tusomavyo katika Qur'an:

Sema: Ni nani aliyeharamisha mapambo ya Mwenyezi Mungu ambayo amewatolea waja wake. Na (nani aliyeharamisha) vitu vizuri katika vyakula? Sema vitu hivyo vimewahalalikia Waislamu(hapa) katika maisha ya dunia (na) vitakuwa vyao peke yao siku ya kiama. Namna hii tunazieleza aya kwa watu wajua(7:32).

Maisha ya Muumini si yale ya kucaa ovyo ovyo na wala si kuishi katika uchafu wa hali zote. Haitarajiwi kujikunyata bali umaridadi wa mavazi, makazi mazuri, elimu nzuri yenyewe manufaa, matibabu, kula na kunywa vizuri. Qur'an inatoa mfano wa Nabii Suleiman(a.s) ambaye Allah(s.w) alimpa utajiri mkubwa. Inaelezwa mali, kasri la kitajiri na kazi zake za sanaa kama ifuatavyo:

“Na kwa Suleiman(tukatiisha)upepo(uliokwenda safari yake ya asubuhi (mwendo wa) mwezi mmoja na safari yake ya jioni) wa mwezi mmoja. Na tukamnyunyizia Chem Chem. Ya shaba. Na katika majini(kulikuwa na) waliofanya kazi mbele yake kwa idhini ya Mola wake. Na kila anayejitenga na amri yetu mionganii mwao Tunamuonjesha adhabu ya moto uwakao. Walikuwa wakimfanyia apendalo kama ngome, masanamu na mabunguu makubwa kama mahodhi na masufuria makubwa sana yasiyoondolewa mahali pake. Tukawaambia: Fanyeni amali nzuri enyi watu wa Daud kwa kushukuru(neema mlizopewa). Na ni wachache wanaoshukuru katika waja wangu.(34:12-13).

Katika sura nyingine, Qur'an inasema hivi:

“Akaambiwa liingie jumba(langu)”(Malkia) alipoliona alidhani ni eneo la maji, akapandisha nguo mpaka katika miundi yake(ili ayavuke hayo maji(Suleiman) akasema hakika hili ni behewa lililosakafiwa kwa vioo. Akasema(yule Malkia) Mola wangu, mimi nimedhulumu nafsi yangu na sasa najisalimisha pamoja na Suleiman kwa Mola wa walimwengu(27:44).

Mafunzo muhimu yaliyopo hapa ni kuwa utajiri, umaridadi, elimu na neema alizopewa Suleiman zilimvuta Mwanamama Malkia Bilqis katika kumpenda Suleiman na kuikubali dini ya Mwenyezi Mungu hivyo ikamfanya ajilaumu nafsi yake kwa kuishi kifisadi akidhani kuamini Mwenyezi Mungu na kuishi kama atakavyo kungelishusha hadhi yake na kumfanya aishi maisha ya

chini, dhalili. Lingine ni kwamba Suleiman alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mali hizo kubwa kubwa kwani yeye alijuwa kuwa zote hizo zilikuwa neema za mola wetu. Alisema:

“Navipenda vitu vizuri kwa ajili ya kumkumbuka Mola wangu”(38:32)

Hapa Qur'an inatubainishia mtazamo wa Suleiman juu ya neema. Mfano wa Suleiman unatuhakikishia kuwa kuchuma na kumiliki mali ni mambo yaliyohalalishwa maadamu tu mali hizo ziwe nyenzo za kumuabudia Allah. Kwa hiyo waumini wanatakiwa kutafuta na kutumia mali kama atakavyo Allah. Mali ni neema za Mwenyezi Mungu(s.w) hivyo itakuwa busara kwa wale walionazo kuzitumia vile anavyoamrisha mwenye neema zake(Allah). Kama mali hazitazamwi kama neema za Allah basi hapo ndipo penye ufisadi. Qur'an inatoa mifano mingi ya jinsi wale waliokengeuka wanavyoitazama mali. Mmoja wa watu hao ni Qarun. Huyu alikuwa tajiri aliyekufuru:

“Hakika nimepewa haya kwa sababu ya elimu yangu(28:78).

Mtazamo wa namna hii juu ya mali hauwezi kuwakurubisha watu kwa Allah badala yake unawatoa katika njia yake na kuwaondolea imani: (Qur'an) inasema:

“Bila shaka Mwanaadamu anamkanusha Mola wake. Naye anayajua haya ana mapenzi makubwa kabisa ya kupenda mali(100:6-8).

Kwa hiyo, Waislamu hawanabudi kuutazama utajiri kwa maelekezo ya Qur'an na wachume mali kwa lengo la kutafuta radhi za Allah na kuutumikia Uislamu. Lazima wazitamani neema zote za Allah kwa sababu neema hizo

zimeumbwa kwa ajili ya wale wenye imani na Ikhilasi ambao hufanya kila jitihada kumridhisha na kumtumikia Allah.

Daima tuwe wenye kushukuru kwa neema hizi na tuige mfano wa Suleyman(a.s).

“Na tukampa Daud(mtoto anayoitwa) Suleiman, aliye kuwa mtu mwema na alikuwa mnyenyeketu mno.(kumbukeni) alipopelekewa jioni farasi walio kimya wasimamapo wepesi wakimbiapo. Basi akasema “navipenda vitu hivi vizuri kwa kumkumbuka Mola wangu(38:30-32).

Wale wanaoishi kwa Muongozo wa Qur'an, wakiwa na mtazamo uliyoelezwa hapo juu ndio watakaostahiki kuingia peponi. Wameishi vizuri duniani na wataishi vizuri zaidi akhera. Zaidi ya raha na starehe zake ziburudishazo nyoyo na macho, maisha ya Akhera yanaongezwa na sifa ya umilele.

Watu wenye mtazamo wa Suleiman juu ya starehe za dunia ndio watakaofaidi starehe za Akhera. Kwa hiyo basi tunapoyatazama maisha ya Akhera kwa wale watakaofaulu ndiyo yenyre starehe za kila namna vivyo hivyo lazima tuwe na mtazamo huwo juu ya maisha ya Ulimwengu ambayo ni sehemu ya maandalizi ya maisha ya Akhera. Badala ya kuchukulia utajiri, starehe na burudani zenyenye kuzingatia mipaka ya Allah kama ni ujisadi waumni hawanabudi kujua kuwa kila neema ni takrima ya Allah waithamini, waifaidi kwa namna bora na washukuru kwayo. Neno takrima kwa asili na usuli wake, lina sifa tu ya wema na ukarimu na halijakuwa na ila ya rushwa wala shere ya mtu kumnumuna mwengine kama wafanyavyo wafadhili au wahisani wa kisiasa.

Sura ya Tatu

Ramani ya Maisha ya Peponi

Kama lilivyo umbile la ulimwengu lenye maumbile kadhaa zikiwemo sayari, nyota, miezi na mengineyo, Pepo na Moto ni sehemu ya maumbile halisi makubwa kabisa ya umbile halisi la Akhera. Mwenyezi Mungu ameujaalia uhai wa mwanaadamu kuwa wa namna mbili. Uhai wa muda mfupi yaani wa ulimwengu huu wa maisha ya mtihani, na uhai wa dumu daima huko Akhera wa maisha halisi ya raha za kufaulu Peponi au adha na taabu za kufeli, Motoni.

Katika Qur'an Mwenyezi Mungu anayaelezea maisha halisi mazuri yenye starehe timilifu na yenye kudumu milele. Yule mtu asiyequwa kima cha starehe hii au asiyequwa namna Qur'an ilivyoelezea starehe hii yumkini itamwia vigumu kupata picha ya Pepo na aina ya maisha yaliyopo huko. Mafundisho haya yanawasimulia watu habari za Pepo ambayo Mwenyezi Mungu amewazawadia. Yanataja neema kubwa kubwa zilizomo humo na yanaelezea starehe zake kwa kila mtu. Yanawataarifu kuwa Pepo ni aina mojawapo kati ya aina mbili za maisha yaliyoandaliwa kwa ajili yao katika ulimwengu ujao na kwamba kila kilicho kizuri kila kistareheshacho, kila kiburudishacho kitakuwa mali yao kwa kiasi ambacho kipo nje ya uwezo wa kufikiri tulionao.

Mafunzo haya yanabainisha kuwa Peponi ni mahali ambapo neema zimeumbwa kwa ukamilifu na ambamo watu wataneemeshwa kila kitu ambacho roho na nyoyo zao zitakitamani na ambamo watu watakidhiwa kila haja na wataondoshewa kila shaka na huzuni, kila dukuduku na sononeko. Kila aina ya starehe na kila neema ipo peponi na itatolewa kwa ukamilifu ambao hapo kabla hakuna aliyeuona wala kuujua Mwenyezi Mungu ameziandaa neema hizo kama zawadi ambazo zitatolewa kwa wale tu anaowaridhia. Mafunzo haya yanaelezea

kila kitu na kila jambo la Peponi. Kwa mujibu wa Qur'an, hivyo usomapo mistari hii jaribu kujenga picha ya mahala hapo pema, kumbuka kwamba Qur'an ni ukweli mtupu, kwa kuzingatia hilo tutafakari ubora wa makazi hayo halisi yanayotusubiri na tufanye kila jitihada ili ustahili kuyapata. Elewa kwamba Mwenyezi Mungu anakupa vyote hivi kwa rehma zake na vitakuwa vyetu moja kwa moja. Sasa iwapo bado tunashindwa kuhiyari kupata neema hii ya starehe za milele basi tukumbuke kuwa chaguo lililobaki ni jahanam ambamo mmejaa mateso ambayo daima itakuwa hofu, huzuni, majonzi, masikitiko na majuto.

Neema na Israfu

Katika jamii za leo watu wengi wana mawazo na hisia lizofichikana vichwani mwao, kwa vile mawazo na hisia hizo ndizo zinazosababisha wabuni dhana, badala ya kuziita dhana za sayansi au tekinolojia kana kwamba ni elimu ngeni isiyopata kuwako kabla. Katika mafundisho ya Qur'an tunaelezwa kuwa Pepo kama mahala bora kabisa penye starehe, kwamba maisha ya humu ni ya raha tupu na utulivu. Watu wengi hivi leo, maisha kama hayo kwa hapa duniani huonekana si ya kiislamu. Haya ni matokeo ya kuyatenganisha maisha hayo na Mwenyezi Mungu katika mafundisho yake ya "kiroho". Hivyo kwa sababu hii ya uelewa huu wa ndivyo sivyo kuna wakati katika jamii watu wengi hudhani kuwa maisha ya starehe, na ya juu na vyote vinavyohusiana na maisha hayo "si vya kiisalmu". Vitu kama nguo za bei kubwa, chakula bora, burudani, dhifa, majumba mazuri, mapambo na kazi nzuri za sanaa huonekana kama ni vitu vya kijahili na huviondoa katika maisha ya kiislamu. Ni vizuri na ni halali kuishi kwa viwango vya juu lakini bila ya kupoteza daraja za misingi, nguzo, faradhi na sunna za dini yetu

Mara nyingi huyaита maisha yaliyojaa vitu hivi kuwa ni ya kifisadi na kuwashutumu wale wanaoishi maisha hayo huku wakizitaja jamii zinazoishi maisha hayo kama ni jamii zilizokosa murua. Neno "safahati" linatokana na neno safihi ambalo hufasiriwa kama ukosefu wa murua, ulevi wa maisha, utovu wa

akili unaotokana na kuishi maisha ya utajiri na starehe na ambavyo sivyo. Maisha ya peponi ambayo Mwenyezi Mungu amewapendelea zaidi waja wake ina kila aina ya raha, starehe na umakinifu, yote haya ni maisha yanayokwenda sanjari na mafundisho ya dini ya Allah.

Watu hawawi mafisadi kwa sababu ya nguo nzuri, majumba mazuri, mazingira yenyeye mapambo na utajiri wa mali. Kama watu wana maadili ya Qur'an na imani nzito wanaweza kuishi wakiwa matajiri wakubwa kabisa bila yakuwa mafisadi, kwa vile wao wanakitazama kila kitu kwa mafundisho ya kiislamu, wao huiona starehe yote inayowazunguuka kama neema, upendeleo na mitihani. Kwa maneno mengine wanatambua kuwa vitu hivi ni hidaya kutoka kwa Allah(s.w), kwahiyio wao humshukuru Mwenyezi Mungu kwa utajiri, starehe, mali na hadhi aliywapa na tangu hapo neema zote zimeumbwa kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Iwapo tutatumia njia ya tafakuri katika jamii zetu za leo, basi tutasema tu kuwa wale wanaoishi maisha ya ujisadi wamekengeuka kwasababu wao hawaoni kuwa jitihada zao pia ni neema kutoka kwa Allah(s.w). Kama wangelizitazama neema hizi kama ni neema basi mtazamo huo ungewapelekeea kumshukuru Mwenyezi Mungu na kisha kuzitumia neema hizo kama Allah alivyopanga au alivyokusudia, wakiepuka israfu na wakizitumia kwa utaratibu anouridhia. Kwahiyio basi utajiri waweza kuainishwa kwa namna mbili baadhi ya matajiri ni waumini wanaozihesabu mali zao zote kama neema kutoka kwa Allah wakati wengine hukengeuka kwa kudhani kuwa zile mali zote walizonazo ni za kwao, wakimsahau Mwenyezi Mungu na hivyo kutumbukia kwenye ujisadi. Tukumbuke, kigezo ambacho Allah amekiweka kutupima waja wake imani ni mali, utajiri na umasikini.

Hali ya Wanaomcha Mwenyezi Mungu

Qur'an inasema kuwa waumini ni wale wanaosema:

“Mola wetu ni Mwenyezi Mungu”, kisha wakenda mwendo mzuri, hao huwateremkia malaika, Msio gope wala msihuzunike, na furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa”(41:30).

Pia Qur'an inasema kuwa waumini wanajua kuwa:

“Hatuikalifishi nafsi ya mja ila kwa kiasi cha uweza wake, hao ndio watu wa Peponi. Wao watakaa humo milele(7:42).

Waumini huamini kudra kwamba Allah hufanya na kutimiza kila jambo. Hivyo huliridhia kila jambo liwatokealo kuwa linatoka kwa Allah kama isemavyo aya hii:

“Sema; halitusibu ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu”(9:51).

Kwa vile wanaotaka kumridhisha Allah, husema:

“Mwenyezi Mungu anatutosha. Naye ni mlinzi bora kabisa. Basi wakarudi na neema za MwenyeziMungu na fadhila(zake), hakuna ubaya uliowagusa na wakafuata yanayomridhisha Mwenyezi Mungu(3:173-174).

Lakini kwa vile hapa duniani ni mahali pa mtihani, Waumini watakabiliwa na matatizo kama njaa, ugonjwa, kukosa usingizi, ajali au hasara ya mali. Wanaweza hata kupata mitihani migumu zaidi kama umasikini na hali ngumu kama isemavyo aya hii:

“Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali ya kuwa hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowafika) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na waliaoamini

pamoja nao wakasema “Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini? Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu(2:214).

Mitihani hiyo haikuwayumbisha Mitume na waumini kutokana na ile imani yao thaabiti juu ya Mola wao na kutokana na ile dhamiri yao ya kuitekeleza Qur'an. Mwishoni mwa aya hiyo, Allah (s.w) anawaahidi Waumini kuwa msaada wake upo jirani nao. Katika aya nyingine Allah (s.w) anasema:

“Na Mwenyezi Mungu atawaokoa wale wamchao kwa ajili ya kufuzu kwao. Hautawagusa ubaya wala hawatahuzuni(39:61).

Hivyo, Waumini wote wanajua kuwa matatizo, shida na taabu zote zimeumbwa kwa minajili ya kuwatahini imani zao na kama ni wenye subira na wanyenyekevu, matatizo hayo yatawapa fursa nzuri ya kukomaa kiimani. Isitoshe mitihani hiyo ndiyo itakayowapatia malipo ya milele katika maisha ya Akhera. Kwa sababu hiyo, watayakabili matatizo hayo hadi kupata tena hali bora, furaha na raha. Katu matatizo hayo hayatoteteresa msimamo wao wala kuathiri hisia na dhamiri zao. Kinachotakiwa ni ibada ya subira.

Badala yake hamasa yao itazidi kuongezeka kwani wanajua kuwa watapata ujira wao kwa ile subira na ule unyenyekevu wao mbele ya Mola wao. Kwa upande wa makafiri mambo yako kinyume na hivyo. Wale wanaokanusha Qur'an hutaabika na adha za rohoni(hupata mateso ya moyo) sambamba na adha za kimwili ambazo huzipata katika maisha ya Dunia hii.

Khofu, huzuni, kukata tamaa, roho juu, wasi wasi, mfadhaiko, kuhamanika, kusononeka, woga na hisia mbaya nyinginezo watazongwa nazo hapa hapa na ambazo ndizo mwanzo wa taabu za motoni.

Mwenyezi Mungu anawaelezea watu hawa katika aya ifuatayo:

“Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu kamuongoza humfungulia kifua chake Uislamu na yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumuhukumu kupotea, humfanya kifua chake kizito, kinaona taabu kubwa(kufuata Uislamu); kama kwamba anapanda mbinguni, Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wale wasioamini(6:125).

Lugha ina mambo. Vipofu wa baadhi ya nchi hujiita **wasioona**. Upofu si tusi wala si ila. Ni majaaliwa kama urefu, ufupi, uwete, uziwi nakdhalika. Neno **Kafiri** nalo si tusi. Ni mtu aliyekufuru. Aliyemkana Allah (s.w). Ama yule ambaye Mwenyezi Mungu kamwongoza ni yule aliyejitanguliza kumcha na kumnyenyeka muumba wake. Akaomba aongozwe Naye. Kila aombaye hujiombea nafsi yake. Mwenyezi Mungu hapendelei, habagui.

Mwenyezi Mungu hapa Anabainisha kuwa ye ye hupenda kuwasamehe madhambi na makosa yao wale wanaomuelekeea kwa unyenyekevu na taadhima na kwamba waja wanaoamini na kutubia, ye ye atawapa neema nzuri nzuri katika maisha haya ya dunia na watapata radhi zake kama isemavyo Qur'an:

“Na ili muombe msamaha kwa Mola wenu kisha mtubie(mrejee) kwake. Atakustarehesheni kwa starehe nzuri kwa muda maalum. Na Akhera atampa fadhila yake kila mwenye fadhila. Na kama mtakengeuka basi nakukhofieni adhabu ya hiyo siku kubwa(11:3).

Kwa maneno mengine, kuomba msamaha kwa Allah (s.w) na kumuelekea Yeye katika kuomba toba ni mionganini mwa mambo yaliyoamrishwa kwa Waislamu wote. Mambo haya yanaonesha jinsi waumini wanavyojitambua kuwa wao hawana uwezo wowote bali ni viumbe dhaifu tu mbele ya Allah (s.w). Wanatambuwa upungufu na kasoro walizonazo kama viumbe na hivyo wao sio maasumu. Hivyo wanaomba rehema za Allah (s.w). Kama alivyosema Mola

wetu, Yeye huwalipa waumini kwa maadili yao mema na kuwapa maisha mema hadi kufa na baada ya kufa kwao.

Katika aya hii Mwenyezi Mungu Anayelezea hivi maisha ya Waumini katika Dunia hii:

“Na wanapoambiwa wale wanaomcha Mwenyezi Mungu: Ni nini Aliyoteremsha Mola wenu? Husema (Ametuteremshia kheri(kutuambia kuwa) wale waliofanya wema katika dunia hii watapata wema, hakika nyumba ya Akhera ni nzuri kabisa na ni bora kabisa, hiyo ni nyumba ya WachaMungu.(16:30).

Pale starehe zote zinapolinganishwa na zile za Akhera,za Dunia hii, huonekana upuuzi mtupu. Kwa hiyo kama ni kuchagua, basi ya kuchagua ni maisha ya Akhera. Mwenyezi Mungu Huwazidishia neema wale waumini ambao tayari wamezielekeza nyoyo zao katika maisha yajayo.

Katika swala zao, Waumini hao huomba maisha mema ya Akhera na pia humuomba Allah (s.w) maisha mema ya hapa Duniani. Mifano ya maombi hayo inatolewa katika aya zifuatazo:

“Mola wetu! Tupe mema duniani na tupe mema Akhera na utulinde na adhabu ya moto(2:201).

Waja wa Allah (s.w) wanaomuamini kwa Ikhlaswi ndio wanaotajwa kuwa Makhalifa wa dunia hii.

“Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini mionganoni mwenu na kufanya vitendo vizuri kuwa atawafanya Makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya Makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini

Atawasimamishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri zetu(24:55).

Sura ya Nne Habari Njema Kwa Wamchao Mwenyezi Mungu

Katika sura ya kwanza tulielezea kuwa waumini wenyе iklasi wanaojitupa kwa Allah (s.w) watafaidi neema zake katika Dunia hii kabla ya kuingia peponi. Moja ya neema hizo muhimu ni miadi ya habari njema ya Pepo. Aya kadhaa zinaizungumzia ahadi hii ya Allah (S.W);

“Wao wana mema katika maisha ya duniani na katika Akhera. Hakuna mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu, huku ndiko kufuzu kukubwa” (10:64).

Nyoyo za waumini zinahamasika kwa habari hii njema kwamba amali zao zitapata malipo mbele ya Allah na kwamba neema wanazozisubiri zipo jirani tu na zimejaa uhondo juu ya uhondo.

Qur'an pia inasema kuwa waumini watapata habari njema kutoka kwa Malaika. Wale waja wanaomuamini Allah kikwelikweli pasipo kumshirikisha na chochote na ambao wanatii amri na mawaidha ya Qur'an na ambao wanaishi maisha yao kwa kufuata mafundisho yake, wao hufurahia kwa matumaini habari hii njema.

Kwa hakika habari hii ni furaha isiyoelezeka kwa waumini wote wanaotumai kuingia peponi kama tunavyosoma katika Qur'an:

“Wale wanaosema: Mola wetu ni Allah na kisha wakashika njia. Hao Malaika huwashukia na kuwaambia, msikhofu wala msihuzunike bali pokeeni habari njema za Pepo mliyoahidiwa”.(Fussilat,30-32)

Allah (S.W) Aliwapa Manabii kazi ya kutangaza habari hii njema. Mwenyezi Mungu Anamuamrisha Mtume (S.A.W) kutangaza kuwa, waumini watapata ujira mkubwa kutoka kwake (Ahzab.47).

Katika Surati Yasin, aya ya 11, inabainishwa kuwa wale walio tii Qur'an na kumuogopa Mwingi wa Rehma watapata msamaha na ujira mkubwa kutoka kwake. Aya ya 17 ya surat Az Zumar inasema kuwa wale wanaoepukana na ibada ya miungu bandia na kumuelekea Allah (S.W) wapashwe habari njema. Na katika surat Yunus aya ya 2, Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume wake, awape habari njema wale wanaoamini kwamba wanayo malipo makubwa mbele yake. Tunapozitazama sifa za wale walioelekezwa katika aya hizo, tunaona kuwa hao ni wale waumini wa kweli walio karibu mno na Mola wao, wanaotambua nafasi zao kama binaadamu na wanaotii maamrisho ya Qur'an na ya Mtume (S.A.W) na wanaomuogopa Allah (S.W).

Ahadi ya Allah

Wale watakaosimama mbele ya Mwenyezi Mungu hali ya kuwa ni waumini, Allah Anawapa ahadi ya Pepo, humo watakaa milele. Na hapana hata chembe ya shaka kuwa ahadi hii itatimizwa, na wale waumini wenye yakini, katu hawana shaka na ukweli huu. Isitoshe ikiwa wao wamezisalimisha nafsi zao Kwake, wanatumai kuwa madhambi yao yatasamehewa na wataruhusiwa kuingia Peponi. Aya ifuatayo inabainisha hili;

“Isipokuwa wakitubu na kudumu kuamini na kufanya yaliyo mema. Hao wataingia peponi wala hawatadhuluiwa chochote. Pepo za milele ambazo (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema amewaaahidi waja wake katika siri (yake). Bila shaka ahadi yake ni yenye kutimizwa (19:60-61).

Ipi? Uwapi Ukweli kuwa Allah Amewaaahidi waumini Pepo, unawapa furaha na kuwatia hamasa isiyosemeka. Wao wanajua kuwa Allah Ameweeka Pepo kwa ajili ya waja wake waliomuamini na kwamba amewafanya wao kama warithi wa Pepo hiyo. Hapa ipo aya nyingine inayoelezea ahadi hiyo; Je mtu yule tuliyemuahidi ahadi nzuri tena atakapoipata atakuwa sawa na yule tuliyemnufaisha kwa maisha ya duniani tu, kisha siku ya kiama awe mionganoni mwa watakaohudhurishwa Motoni? (28:61). Iwapo Allah amewaaahidi Pepo waja wowote wale wenye kumcha, basi hao watapata neema za milele kwa rehema zake. Na pale waumini watakapoingia Peponi, watatoa shukurani zao kwa kusema hivi;

“Nao wasema Alhamdulillah (sifa njema na shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye Ametutimizia ahadi yake na Ameturithisha ardhi(ya huku peponi), Tunakaa katika mabustani haya popote tupendapo “Basi ni malipo mazuri yaliyoje ya watendao (memma), (39;74).

Waumini ambao wamepewa habari njema wakati wa maisha ya Dunia ambao Allah (S.W) Amewaaahidi Pepo ya maisha yao haya ya dunia watapata kile walichotumai kukipata. Hatimaye wakati huo uliosubiriwa kwa muda mrefu utafika, wataingia pale mahala pema palioje na mafikio bora kuliko mafikio yoyote. Katika maisha yao yote walikuwa wakiomba kupata na walijitahidi kwa kila hali ili wastahiki kuingia. Ni pahala penye kila kitu, palipoandaliwa kwa ajili ya waumini na milango yake iko wazi kwa ajili yao. Aya ifuatayo inatoa picha ya jinsi watakavyoingia peponi. Mabustani ya milele wataingia wao (pamoja) na

waliofanya mema mionganini mwa wazee wao na wake zao na kizazi chao. Na Malaika watakapoingia katika kila mlango wanawasalimu,

“Salamun Alaykum”, iwe amani juu yenu, kwa sababu mlisubiri. Basi ni mema yaliyoje matokeo ya nyumba ya Akhera kwa wanaomcha Mungu (13:23-24).

Watakaribishwa Peponi kwa salamu za amani na heshima, hao ndio watakaolipwa ghorofa (za peponi) kwa kuwa walisubiri, na watakuta humo heshima na amani (25:75).

“Na hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu watakuwa katika mabustani na chem chem.,yaingieni salama usalimini”(15:45-46).

Sasa kimebaki kitu kimoja nacho ni kuziona starehe za hayo makazi ya milele waliyoandaliwa waumini na kutunukiwa kila aina ya neema. Allah (S.W) amezijaza imani nyoyo za waumini na kuzitia nguvu kwa roho itokayo kwake na atawaingiza katika mabustani yenye mito itiririkayo chini yake, wakae humo milele. Mwenyezi Mungu amewaridhia, hilo ndilo kundi la Mwenyezi Mungu na kwa hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu Amethibitisha kikweli kikweli nyoyoni mwao imani na Akawatia nguvu kwa roho zitokazo Kwake na atawaingiza katika mabustani yapitayo mito mbele yao humo watacaa daima, Mwenyezi Mungu amekuwa radhi nao, na wao wamekuwa radhi Naye.

“Hao ndio kundi la Mwenyezi Mungu. Sikilizeni hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo linaloshinda (linalofaulu)”. (58;22).

Kifo cha Muumini ni chepesi, hesabu nyepesi

Si Waumini wala makafiri wanaoweza kujuwa lini na wapi watakapofia. Ukweli huu unafafanuliwa na Qur'an;

Kwa hakika ujuzi wa kiama uko kwa Mwenyezi Mungu tu; Naye huteremsha mvua (wakati autakao) na Anayajua yaliyopo matumboni (hakuna anayejua isipokuwa Yeye) na nafsi yeoyote haijui ni nini itachuma kesho, wala nafsi haijui itafia ardhi gani. Bila shaka Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi, Ndiye mwenye khabari (ya mambo yote) (31:34).

Pamoja na hayo, Qur'an inatuarifu kuwa jinsi mauti yatakavyowajia waumini, namna roho zao zitakavyotolewa na nini kitakachotokea kwao wakati wa sakaratinauti. Tunavyofahamishwa hapa ni kuwa waumini huyaonja mauti kwa kutolewa roho kwa ulatifu. Pale waumini wanapokufa roho zao huchukuliwa kutoka Duniani na kupelekwa makazi mengine. Mwenyezi Mungu Anaielezea safari hii nyepesi katika Surati An-Nazi'ati, aya ya 2 ambapo Anawataja wale Malaika watoao roho kwa upole. Aya nyingine inatuambia kuhusu mazungumzo ya Malaika pale wanapokuja kuchukua roho ya Muumini.

Wale ambao Malaika huwafikisha katika hali njema wakasema “Amani itakuwa juu yenu, ingieni peponi kwa sababu ya yale mema mliyokuwa mkiyatenda (16:32).

Aya ifuatayo inaeleza kifo cha Muumini: hautawahuzunisha huo mtaharuki mkubwa, na Malaika watawapokea (na kuwaambia) “Hii ndiyo ile siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa (21:103).

Ni dhahiri kuwa, Waumini ambao wameishi maisha mema katika Dunia hii watakuwa na kifo kizuri na chepesi na maisha yao ya ulimwengu ujao, huanza

pale pale wanapofikiwa na Malaika. Tokea hapo na kuendelea, uhusiano wao na Dunia utasita (utakoma) na watapelekwa mahala walipopangiwa ambapo kutoka huko watakuja mbele ya Mwenyezi Mungu. Baada ya roho za Waumini kuchukuliwa kwa upole na Malaika sasa inakuja awamu ya hesabu za amali pale watu wote watakopokusanyika mbele ya Mwenyezi Mungu wakiwa na yale waliyoyatenda. Mlolongo wa matukio ulioanza siku ile ya kufufuka utaendelea kwa kila mtu kufufuka akiwa na kiwiliwili kipyga na kukusanyika ukingoni mwa moto wa Jahanamu. Baadaye mashahidi wote wataletwa ndani.

Daftari la amali la kila mtu litafunguliwa na kila mtu atahesabiwa kulingana na kile alichofanya Duniani. Baada ya hapo Waumini wote watanusurishwa na moto wa Jahanamu kwa rehema za Mwenyezi Mungu na kuingizwa Peponi. Qur'an inaelezea hatima ya Ulimwengu na hali ya Waumini siku hiyo katika aya kadhaa. Mwisho wa Dunia utakuwa pale litakapopigwa baragumu la kwanza. Dunia na Ulimwengu utahilikishwa na kubomolewa moja kwa moja. Milima itavunjwa vipande vipande, bahari zitawaka moto na mbingu zitaondoshwa. Litakapopigwa baragumu la pili watu wote watafufuliwa na kukusanywa mahali pamoja kwa ajili ya kuhesabiwa amali zao. Kila walichokifanya hata kiwe kiduchu kiasi gani kitaleta hizaya kwa Makafiri. Lakini furaha na raha tupu kwa Waumini, kwani Mwenyezi Mungu Anaielezea siku hiyo kuwa ni siku ambayo Allah hatomdhililisha Mtume na walioamini pamoja naye;

Enyi mlionamini tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli; huenda Mola wenu Akakufutieni maovu yenu na kukuingizeni katika Pepo zipitazo mito mbele siku ambayo Mwenyezi Mungu hatamdhililisha Mtume (S.A.W) wala wale walioamini pamoja naye; nuru yao itakuwa inakwenda mbele yao na pande zao za kulia na huku wanasesma; Mola wetu! Tutimizie nuru yetu, na utughufirie, hakika wewe ni mwenye uwezo juu ya kila kitu (66:8).

Mwenyezi Mungu anaahidi; Bila shaka sisi tunawanusuru Mitume wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi (kushuhudia amali za viumbe) (40;51).

Siku ya mwisho Waumini wa kweli watapokea daftari na amali za matendo ya Duniani kwa upande wa kulia. Hesabu yao itakuwa nyepesi kama inavyosema Qur'an na watapewa stahiki yao ya kuingia Peponi;

"Basi, ama yule atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa kuume (kulia) atasema (kwa furaha) Haya someni daftari langu (nililopewa sasa hivi). Hakika nilijua kuwa nitapokea hesabu yangu (kwa vizuri, kwani nilikuwa nafanya mazuri). Basi ye ye atakuwa katika maisha ya raha katika Pepo tukufu. Vishada vya matunda yake vitakuwa karibu (vinachumika bila tabu). (waambiwe) kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya vitendo mlivyo fanya katika siku zilizopita (69;19-24).

Waumini wanapata kile alichohahidi Mwenyezi Mungu, watafurahi siku hiyo; (waambiwe) "ingieni (peponi) kwa salama". Hiyo ni siku ya kukaa daima (katika starehe za huko Peponi) (50;34).

Na hali yao inaelezwa hivi; Ama atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kulia, basi ye ye atahesabiwa hisabu nyepesi. Na atarudi kwa watu wale, hali ya kuwa ni mwenye furaha. (84;7-9)

Pale watakapopewa hesabu yao, Waumini watajawa na furaha ya kunusurika. Aya inasema; "Yaingieni salama, usalimini (kwa salama na muwe katika amani) (15;46)

Hili pia linaelekezwa katika aya nyingine:

“Ewe nafsi yenyе kutua! Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika na Mwenyezi Mungu aridhike na wewe. Basi ingia katika kundi la waja wangu (wazuri) uingie katika Pepo yangu (89:27-30).

Hapo basi, Mwenyezi Mungu Amewasamehe madhambi yao wale waja waliowapa rehema na kuyabadili mabaya yao kuwa mema na kuwapa ruhusa ya kuingia Peponi.

Waja hawa wanasema; Akaambiwa “Ingia Peponi”. Akasema, laiti watu wangu wangejua (haya niliyoyapata) wangejua jinsi Mola wangu Alivyonisamehe na Akanijaalia mionganoni mwa walioheshimiwa (36:26-27)

Katika aya nyingine, Mwenyezi Mungu anatangaza habari hii njema kwa watu wa Peponi; Mwenyezi Mungu Atasema:

“Hii ndiyo siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata bustani zipitazo mbele yake mito. Humo watacaa milele. Mwenyezi Mungu Amewawia radhi; nao wawe radhi naye. Huku ndiko kufaulu kukubwa (5:19).

“Enyi waja wangu (mlio wazuri)! Hamtakuwa na khofu siku hiyo wala hamtahuzunika (43:68) Katika aya nyingine Allah Anatutaarifu Na Pepo italetwa karibu kwa wamchao Mwenyezi Mungu, haitakuwa mbali nao (50:31)

Sura ya Tano Mandhari ya Pepo na Uzuri wake

“Mfano wa pepo waliyoahidiwa wamchao Mwenyezi Mungu (ni hivi); mbele yake inapita mito, matunda yake ni ya daima na (pia) kivuli chake. Huu ndio mwisho wa wale wamchao Mwenyezi Mungu. Na mwisho wa makafiri ni moto (13:35).

Uzuri wa mandhari ya Pepo yenye rangi ya kijani kibichi ni mionganini mwa neema za kupendeza za Peponi. Aidha, maghorofa yaliyojengwa mabustanini yakiwa na mito mbele yake ni mapambo ya Peponi. Humo hamna jua kali wala baridi kali.

“Humo wataegemea viti vyakie enzi, hawataona jua kali wala baridi kali. Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yake yataning’inia mpaka chini. (76:13-14).

Pepo ina hali hiyo ya hewa ya kupendeza, kwamba humo hakuna mtu atakayekosa raha. Pepo haina joto kali wala baridi kali. Katika Pepo Mwenyezi Mungu Atawaingiza waumini katika vivuli vizuri kabisa;

“Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, tutawaingiza katika mabustani yapitayo mito mbele wakae humo milele. Humo watakuwa na wake walioamini na tutawaingiza katika vivuli vizuri kabisa (4:57).

Usemi huu “vivuli vyakie enzi” mbali na kubainisha kuwa hali ya hewa itakuwa ya kustarehesha kama vile mtu atakavyotaka pia unaonesha kuwa mazingira na hali ya Peponi vimesaniwa kwa namna ya kuipa nafsi ya

mwanadamu raha na starehe kamili. Kila kitu na kila hali katika pepo kitakuwa vile atakavyo muumini. Mojawapo ya starehe za mandhari ya Peponi ni mtiririko wa maji;

“Na maji yanayomiminika (kwa vizuri) (56:31)”

Kama tuonavyo katika maisha haya, nafsi ya mwanadamu huburudika inapoona maji yatiririkayo katika mito, maziwa, chemchem na vijito vinavyotiririka mwituni. Vyote hivi vinaburudisha nafsi ya mtu. Mabwawa ya kuchimbwa, mashamba, mabustani pamoja na vijikondo vya asili vyote vinatengenezwa kutokana na raha hiyo ya nafsi. Vitu hivyo huistarehesha nafsi. Sababu kuu ya vitu hivyo kuleta raha kwa binadamu ni kwamba nafsi ya mtu imeumbwa kwa ajili ya pepo. Starehe hizi zinalezwu hivi; “Humo mna chem chem mbili zinazotoka maji kwa nguvu.” (55:66).

Kuyatazama maji na kusikia mvumo wa maji yanayotiririka nako kwaustarehesha na kuuburudisha moyo wa mtu. Kule kuyaona na kuyasikia maji yanavyobubujika kutoka juu kunaleta raha na ni mojawapo ya neema ambazo watu wamshukuria na kumtukuzia Mwenyezi Mungu.

Hasa hasa maji yanapotiririka kutoka milimani katikati ya miti au juu ya mawe kwa kweli yanapendeza kuyatazama na hata pale yanapomwagika na kujikusanya kutengeneza bwawa. Daima maji yanayotiririka ni ishara ya starehe kubwa isiyochosha. “Na hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu watakuwa katika mabustani na chemchem (zinazopita mbele yao)” (15:45).

“Bila shaka wamchao Mungu watakuwa katika vivuli na mito.”
(77:41)

“Vivuli ni sehemu makhpususi zilizoumbwa ili waumini waweze kukaa na kupata starehe yote hiyo (Allahu A’alam). Na kuhusu maghorofa, vivuli hivi pia vina wekwa mahala pa juu ili watu wa peponi waone mandhari yao wakiwa juu na watazame vyote vilivyomo. Vivuli hivyo vinaleta raha na starehe makhpususi kwa waumini. Watu wanapewa vyakula mbalimbali na matunda ya aina kwa aina na wanakabiliana kufanya maongezi kwa furaha. Tena mbele yao kuna mito ambayo inaiburudisha nafsi ya binadamu na kuwaongozea mvuto machoni mwao. Katika mito hiyo yanatiririka maji matamu.

Starehe nyingine ni malisho yaliyomo kwenye mabustani, kwa mfano; Sura ya 42, Aya ya 22 inasema; “Na wale walioamini na kutenda mema watakuwa katika mabustani ya Peponi; watapata watakayoyataka kwa Mola wao hiyo ndiyo fadhlila kubwa. Vyote vilivyomo humo ni kwa ajili ya waumini tu. Moja kati ya mambo yaliyomo humo ni mandhari yenyenye mseto wa vivutiyo. Humo mna mimeya inayostawi bila kukauka, mimeya yenyenye harufu nzuri na mna aina ya wanyama tunaowajuwa na tusiowajuwa. Mabustani haya yanapambwa na matunda ya aina mbalimbali na miti mbalimbali na nyanda zenyenye majani ya kijani kibichi;

“Yenye rangi nzuri ya kijani kilichowiva (barabara).” (55:64)

Yana mimeya na maua na mahali pengine pana mabwawa na mabubujiko; “Watakuwa katika vivuli vya mikunazi isiyio na miba. Na migomba iliyopangiliwa vizuri na kupangiliwa mazao yake.” (56:28-29).

Kwa kuzingatia vitu vyote hivi tunaweza kujenga picha ya jumla ya Pepo. Baadhi ya sifa zake zinatukumbusha vitu vilivyopo hapa duniani na neema nyingine ni za aina yake, zina starehe za aina yake ambazo hakuna mtu yeoyote ambaye amewahi kuziona au hata kuzisikia na kwamba hata akili zetu haziwezi kuzifikiria au kuzielezea.

Lazima tufahamu kuwa vitu hivi vizuri na raha za aina kwa aina zinawasubiri waumini. Hivi vimeandaliwa kwa elimu ya Allah isiyo na ukomo na iliyo NJE ya akili zetu. Kama inavyosema Aya 22 ya Suratil-As-Shura, watapata kila wanachokitamani kwa Mola wao. Hii ni neema kubwa. Kila kitu Peponi, pamoja na starehe zake, kimeumbwa kwa kuzingatia utashi na raha ya muumini. Kwa maneno mengine Allah (S.W) huzechia hisia za muumini kazi ya kuyajenga mazingira ya Peponi ikiwa ni rehema yake.

Raha isiyo na mwisho

(Waambiwe); kuleni na kunyweni kwa furaha kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyatenda. (77:43).

Qur'an imetangaza kuwa watu wa Peponi watastareheshwa kwa kila watakachokitamani vikiwemo vyakula vitamu na vinywaji mbalimbali. Huko watu hawahitaji shibe kwani vyakula na vinywaji hivyo vimeumbwa kwa ajili ya kustarehesha tu. Chakula hiki kinafanana na chakula cha dunia hii. Watu wa Peponi wataulezea mfanano huo kwa maneno haya;

“Na wabashirie walioamini na kufanya vitendo vizuri kwamba watapata mabustani yapitayo mito mbele yake; kila mara watakapopewa matunda humo kuwa ni chakula watasema; haya ndio yale tuliyopewa zamani (ulimwenguni). Kwani wataletewa (matunda hayo) hali ya kuwa yamefanana); na humo watapata wake waliotakasika na watacaa milele humo. (2:25).

Vyakula vingi katika dunia vinalika kutohana na hamu ya kula ya watu na vinaleta raha kwa haiba na ladha yake. Allah (S.W), Ameshaviumba vyakula vinavyofanana huko peponi ili kuleta raha kwa waumini. Isipokuwa, tafauti na

vyakula nya Duniani, hapatakuwa na khofu ya kunenepeana, kulimbikiza lehemu mwilini, kuvimbiwa wale, kwani Allah (S.W) atawaambia;

“Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyatenda (77:43).

Kuweza kula na kunywa pasi na kiasi ni neema kubwa inayoleta raha kweli kweli.

Sura ya Sita

Muumini huishi mahali gani Peponi?

Ili kupata Pepo, watu wanapewa mitihani katika maisha ya Dunia. Waumini hufanya juhudhi na bidii kubwa kutafuta radhi za Mola wao. Wanaelekea na kujitupa kwake kwa ikhlasi. Wakimtukuza na kumshukuru wakati wote, wakimuomba Yeye tu na wanatubia kwake. Kwa ajili hiyo Allah huwapa neema za Peponi. Peponi, Allah (S.W) Huwaruzuku waumini kila aina ya matunda na nyama wanayoipenda, nyama zisizosababisha ongezeko la lehemu wala kukifu. Na tangu hapo umbile watakalokuwa nalo halitaruhusu udhaifu kama huo.

“Na Tutawapa (kila namna ya)Matunda na (kila namna za) nyama,kama vile watakavyopenda”(52:22)

Na atawapa nyama yoyote ya ndege wanayoipenda.

“Na matunda(namna kwa namna) kama watakavyopenda. Na nyama za ndege kama watakavyotamani (wenyewe).”(56:20-21).

Isitoshe chakula chao hakitakwisha:

“Hakika hiyo ndiyo riziki yetu isiyomalizika”(38:54).

Waumini wataingia katika Pepo ambamo wataruzukiwa pasipo hesabu.

”Afanyaye ubaya hatalipwa ila sawa na uovu wake,na afanyaye wema akiwa mwanaume au mwanamke naye ni Muislamu,basi hao wataingia peponi waruzukiwe humo bila hesabu”(40:40).

Wataweza kula kwa kiasi wanachotaka, na watakula vyakula vyakula vya aina kwa aina vilivyomo humo. Vyakula hivyo havitapunguwa na hakuna atakayeshindwa kula kwasababu ya shibe au ugonjwa. Matunda ndiyo chakula kilichotajwa sana katika Qur'an. Peponi, Waumini watapata aina kwa aina za matunda wanayotamani.Qur'an inaeleza hivi:

”Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao ,na mashada ya matunda yake yataning'inia mpaka chini.(76:14).

Hivyo tunafahamishwa kuwa matunda ya Peponi yanastawi mitini katika mazingira asilia na kwamba waumini wataweza kuyachuma na kuyala. Surati waqia 28-29 watakuwa katika vivuli vya mikunazi isiyo na miba. Na migomba iliyopangiliwa vizuri mazao yake. Maana yake ni kuwa matunda hayo yanaweza kupatikana kirahisi kwani neema za peponi hazina hesabu. Matunda ni mengi mno matawi ya miti yapo chini chini , hivyo ni rahisi kuyafikia. Matunda haya yatawekwa kwenye vibebeso vya dhahabu na fedha na sahani za kupendeza zilizosaniwa na kunakshiwa kwa ajili ya waumini ambao kila mmoja atakuwa kwenye jumba lake la fahari watakuwa wameketi kwenye viti vya fahari wakizungumza.

Makokwa, makovu ya uozo, makambakamba ambayo husumbua watu pale walapo matunda ya dunia hii vyote havitaonekana ili kuleta raha ya pepo. Matunda yote hayo yanatolewa bure kwa waumini huku yakipendeza machoni mwao na yakiwa hayana upungufu wowote ule. Aidha matunda haya yameongezewa rangi na uzuri kwa ajili ya pepo. Haiba ya miti ya matunda hayo yenye rangi mbalimbali yaleta mvuto zaidi wa mandhari.

Rangi ya kijani ndiyo itakayokoza zaidi na ndani yake itakuwa na rangi ya manjano, rangi ya machungwa na rangi nyekundu. Mchanganyiko huo utaleta haiba maridadi ya kuliburudisha jicho la mwanadamu. Hii ikiwa ni ishara ya usanii mkubwa kwa Allah (S.W) ambao utakuwa sababu ya waumini kumtukuza na kumuhimidi Allah (S.W).

Navyo vinywaji teletele vitakuwa na ladha bora kabisa. Surati As-saaffati, aya ya 43.

Katika bustani za neema. Wako juu ya vitanda[Viti vya enzi vya fahari], wamekabiliana[wanzungumza]. Wanazungushiwa gilasi zenye vinywaji safi. Vyeupe vyenye ladha kwa hao wavinywao; kwa vinywaji hivyo hautokua udhia wala kutokwa na akili. Huko peponi watanyweshwa vinywaji (vizuri) viliyofungwa (kwa vizibo madhubuti).Mwishowe (vinywaji hivyo vinaleta harufu ya) miski .Na katika(kupata) haya washindani wenyewe kushindana.Na mchanganyiko wake ni maji ya Tasnymu .(Hiyo ni) chemchem watakayoonywa(watu) waliokaribishwa na (Mwenyezi Mungu.)(83:25-28).

Kama zisemavyo aya hizi,kile wakinywacho pia hutoa harufu nzuri na ukweli.. Allah (S.W) anasema kuwa vinywaji hivi vitamiminwa katika gilasi. Havitamletea mnywaji maumivu kichwani au kumfanya apoteze akili .Wanaotoa huduma ya vinywaji hivi ni vijana walioteuliwa na Mwenyezi Mungu.

'Mwenyezi Mungu amewaalidi wanaoamini wanaume na waumini wanawake mabustani yenyeye mito mbele yake wakae humo daima na makazi mazuri katika mabustani hayo yenyeye kudumu.Na radhi za MwenyeziMungu ndizo kubwa zaidi.Huko ndiko kufuzu kukubwa (9:72).

Kama tulivyosema mwanzo,makazi ambayo waumini huishi makazi yao ya dunia ni mahali ambapo Allah ametaka pajengwe majumba ambamo jina lake likumbukwe na litukuzwe. (Waonekane kwa kusali nyakati tano) nyakati ambazo Mwenyezi Mungu ameamrisha zitukuzwe na litajwe jina lake Misikitini humtukiza humo asubuhi na jioni(24:36). Makazi ya Peponi yako kama hivyo,ni sehemu zenye starehe nzuri zisizo na kifani ambamo Allah (S.W) hudhukuriwa, hutajwa na kushukuriwa. Kama vile majumba na maghorofa yajengwavyo katika haiba nzuri, ya Peponi yamejengwa mfano wa hayo kwa usanifu na teknolojia bora zaidi. Majumba yaliyotajwa katika Qur'an kwa ujumla yamejengwa kwa rosheni.

”Lakini waliomcha Mola watapata ghorofa zilizojengwa juu ya ghorofa;chini yake hupita mito Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu naye havunji ahadi yake”(39:20).

Maghorofa hayo yaliyojengwa sehemu zenye miinuko, yakiwa na mapambo sehemu zote mpaka chini yakionesa mandhari ya Miji (*cities*) ya kupendeza inayotoa fursa kwa wakazi wake kutazama vitu vingi na vizuri kwa wakati mmoja. Qur'an inabainisha kutakuwa na maji yanayotiririka chini ya maghorofa hayo yaliyojengwa vilimani. Hivyo ili kuyaona mandhari hayo, maghorofa yanaweza kuwa na vyumba maalumu vya kukaa na madirisha yenye vioo katika pande zote nne. Maghorofa hayo yamesaniwa kuiburudisha nafsi ya mwanaadamu kwa raha kemkem. Waumini watakaa kwenye viti vyao vya fahari, wakifaidi matunda na vinywaji vizuri huku wakitazama chini kwa starehe wakiangalia kivutio kimoja baada ya kingine.

Raha za milele za peponi

Kwanza watu wasidhani kwamba Peponi ni kama jumba kubwa, humo watu wamejazana kwa pamoja wakiangalia hiki na kile kwa pamoja wakiwa wamekaa au kusimama. Mandhari ya Peponi ni yale yafananayo na miji mikubwa

yenye shughuli nyingi zisizo na mfano, safi, iliyopangwa vizuri kiujenzi, tangu safu za nyumba na majumba, vichochoro, vijia, njia na barabara. Peponi kuna nyumba, majumba na maghorofa yaliyojengwa na kurembwa kwa nakshi nzuri na rangi mchanganyiko yakiwa na viti vyta burudani na vya fakhari. Waumini watakaa huku wakiwa wameelekeana;

“Watakuwa juu ya viti vyta fakhari viliwyotonewa (viliwyotiwa mapambo). Wataviegemea waelekeane (wanazungumza)” (56:15-16).

“Watakuwa wameegemea juu ya viti vyta fakhari viliwyopangwa safu safu, na Tutawaoza wanawake wanaopendeza wenye macho ya mazuri (Makubwa)” (52:20).

Wale waumini ambao Mwenyezi Mungu amewapa neema za peponi watamshukuru Mwenyezi Mungu. Qur'an inasema; wataingia katika mabustani ya enzi ambamo watavishwa vikuku vyta dhahabu na lulu na ambamo nguo zao zitakuwa za hariri. Watasema Al-hamdulillahi, "Mabustani ya milele watayaingia, humo watapambwa vikuku vyta Dhahabu, na Lulu, na nguo zao humo zitakuwa za hariri. Na watasema (katika kushukuru kwao) sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu aliyetuondolea huzuni, kwa yakini Mola wetu ni Mwingi wa msamaha na Mwenye kushukuru. (35:33-34). Wakiwa wamekalia makochi laini waumini, watatazama huku na kule; "Wakae juu ya viti vyta fakhari wakitazama (starehe zao) (83:23). Watakuwa wakiangalia vivutio na starehe za Pepo na neema kubwa kubwa. Hii itakuwa dhifa yenye uhondo mkubwa kweli kweli kwa waumini.

Waumini watazifaidi starehe na raha hizi kwa pamoja pasipo kujali tofauti ya wakati na zama walizoishi duniani. Hii ni neema inayopatikana peponi tu. Mathalani kutembeleana na kukaa kwenye viti vinavyoolekeana na kuongea na watu mliopendana, uliosikia umaarufu wao kiibada katika zama zao, huku

mkimdhukuru Allah pamoja nao ni starehe ambayo haiwezi kupatikana duniani. Starehe hii ipo Peponi tu.

Peponi, kila kitu wanachotamani waumini kitaletwa kwao na watumishi (matarishi, wahudumu) maalumu walioteuliwa kwa kazi hiyo. Qur'an inatufahamisha;

Iwe wanawapitia watumishi wao wanaopendeza kama kwamba ni Lulu zilizomo ndani ya chaza (ndio kwanza zimepasuliwa) (52:24).

Waumini ambao Allah (S.W) amewaruzuku Pepo ni watu waliochaguliwa na ni watu wenye heshima. Kule kutajwa kwao kuwa wako katika nafasi yenye cheo kunabainisha heshima ambayo Allah amewapa;

“Hao ndio watakaopata riziki maalum. Matunda ya kila namna na wataheshimiwa.” (37:41-42).

Wale waliotajwa punde, ambao wanawahudumia waumini kila watakavyo na kuwapatia huduma muda wote, wametajwa katika Qur'an kama watu wasio badilika kiumri:

“Na watawazunguukiya (kuwatumikia wavulana wasiochakaa, ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizotawanywa. (76:19),

Waja hawa ambao kazi yao pekee ni ku wahudumia waumini vile watakavyo na kwa vile neema zenyewe zinatolewa bure basi uhudumu huo wa daima ni sehemu ya starehe. Vyombo vitakavyotumiwa katika kazi hii ya uhudumu pia vina thamani kubwa na ni bora kabisa; watakuwa wanapitishiwa sahani za dhahabu na vikombe (vyo dhahabu); na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia, na nyinyi mtakaa humo milele (43:71).

Katika dunia hii waumini hupata vitu vingi, baadhi yao wakipata neema karibu kama zile za maisha ya peponi. Tunaweza kuona malighafi bora inayotumika kutengenezea nguo za peponi. Allah anawaagiza watu kuvaan nguo nzuri katika dunia hii kama inavyoelezwa hapa;

(Anasema Mwenyezi Mungu kuwaambia wanadamu wote tangu hao wa zamani huko). Enyi wanadamu! Hakika tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo; na nguo za utawa ndizo bora zaidi. Hayo ni katika ishara (neema) za Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka. (7:26).

Katika Surati A'raf, aya 31, Allah (S.W) anawahimiza waumini kuvaan nguo safi na nzuri;

Enyi wanadamu! Chukuweni mapambo yenu wakati wa kila swala; na kuleni vizuri na kunywensi vizuri. Lakini msipite kiasi. Hakika ye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao kiasi (wapindukiao mipaka).

Kwa hiyo nguo zinazovaliwa peponi zitakuwa bora na maridadi zaidi kuliko zile za duniani. Qur'an hasa hasa inataja aina mbili za malighafi zinazopatikana Peponi, hariri laini na hariri nzito;

Watavaa hariri laini na hariri nzito; wakikabiliana (wanazungumza). (44:53).

Hapa duniani malighafi hizi ni adimu sana, ghali sana na ndizo zenye ubora mkubwa. Uzuri na umaridadi wa vazi hilo utawazidishia mvuto wale wanaolivaa. Ni kweli kuwa malighafi na nguo zinazopatikana humo siyo tu za aina hizo mbili. Kwani Allah (S.W) aliyetoa neema hizi atawavisha watu wa Peponi mavazi mengi maridadi yatokanayo na malighafi nyinezo

nyingi na nzuri nzuri. Anaweza kuumba mitindo ya mavazi na malighafi zisizojulikana katika dunia hii. Qur'an inatuambia kuwa nguo maridadi inayopambwa kwa vito vya thamani huzidisha mvuto. Vikuku vya dhahabu, Fedha na Lulu ndio hasa vimetajwa kama aya hizi;

“Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza wale walioamini na kufanya vitendo vizuri katika mabustani yapitayo mito mbele yake. Humo watavishwa mapambo ya mikononi ya dhahabu na lulu, na mavazi yao humo yatakuwa hariri.” (22:23).

“Juu yao wana nguo za hariri, za kijani kibichi na za hariri nzito. Na watavikwa vikuku vya fedha, na Mola wao atawanywesha vinywaji safi kabisa.” (76:21).

Sura ya Saba Neema na Mapambo ya Peponi

Sifa kubwa ya vitu vya Peponi ni zile raha zake tofauti tofauti na starehe zenyeye mvuto vyote vikiwa ni kazi ya Allah (S.W) yenyeye ujuzi na usanii usio na mfano. Makazi atakayotunukiwa mja aliyefuzu ni nyumba au jumba ambamo mna kila kitu tayari vikiwemo, viti vilivyonakshiwa madini ya thamani na kupangwa vizuri sehemu zilizo juu. Nguo zilizo tayari ambazo zimetengenezwa kwa hariri nzito na hariri laini na kupambwa na vito vya dhahabu na fedha. Katika Qur'an Allah (S.W) ametoa maelezo mengi kuhusu Pepo lakini maneno aliyoyatuma yanawawezesha waumini kupata picha ya jumla kwa kulinganisha na hali yao ya maisha hapa Duniani. Katika Pepo, kila muumini atapata kila alichokihisi, na kwamba huko kuhisi kile atakachokitaka, itakuwa ni neema nyingine aliyyotunukiwa na Allah (S.W). Kwa ufupi atatunukiwa aina zote za neema, vivutio na makazi mazuri vyote vikiwa vimeumbwa kwa makusudio halisi ya kumstarehesha yeye. Vyote avionavyo mwanaadamu katika vyakula, matunda, vinywaji, mavazi ni taswira ndogo tu ya vile atakavyovikuta Peponi. Mbali na neema zilizotajwa katika Qur'an, Allah (S.W) amewaandalia Waumini mengi yaliyo nje ya ufahamu, yasiyojulikana wala kuwa na mfano wake katika maisha haya kama ambavyo Mwanaadamu kabla ya kuja hapa duniani hakuwa akifahamu lolote juu ya maisha haya na vyote vilivyomo.

“.....Wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, tutawaingiza katika mabustani yapitayo mito mbele yake kwaajili ya kukaa humo milele. Humo watakuwa na wake waliotakasika na tutawaingiza katika vivuli vizuri kabisa (4:57).

Peponi ni pahali pema pa maisha ya milele ambapo Allah (S.W) amepaandaa kama malipo kwa waja walioamini kama tulivyoona hapo mwanzo.

Qur'an inaielezea kwa ufupi Pepo kwa kuyataja majumba ambayo watu wataishi humo, chakula na vinywaji watakavyo kunywa, nguo watakazovaa na vitu vizuri vizuri vitakavyokutwa humo. Tofauti na wengi wanavyodhani kuwa peponi kuna maisha ya kiroho, kwa hakika uhai na maisha ya Peponi, baada ya maisha ya ufu ya barzakh, ni uendelezo wa maisha kama haya ya Dunia. Akiwa Peponi Mwanaadamu hataishi kiroho bali ataishi akiwa na umbile lake kamili bali lililobora zaidi ya hili alilonalo sasa. Hata hivyo maisha hayo ni mazuri mno hayawezhi kulinganishwa na haya ya duniani ila kuna mambo yanayolingana. Kutokana na mambo haya, pale waumini wanapoyafariki maisha haya ya dunia na kwenda Akhera huwa hawapati hofu wala ugeni, hiyo ni kusema watayazoea maisha hayo kirahisi tu. Maisha yao mapya ya milele yatakuwa ya kweli kuliko kivuli cha haya waliyoishi hapa. Kwa maneno mengine watakuwa na vyakula na vinywaji bora, nguo maridadi kabisa, majumba mazuri, wake na waume. Kama isemavyo Qur'an, wataingia Peponi pamoja na wanawake ambao Allah (S.W) amewazawadia kama malipo yao na watakaribishwa kwa shangwe na shamra shamra. Kwa wenye fikra dhaifu, bora wakumbuke kuwa mke huolewa na mume huowa

Ingieni bustanini Peponi nyinyi na wake zenu; mtafurahishwa humo (43:70).

**Qur'an inawaelezeya wanawake wa Peponi kama Mahurul-ayn.
Mbali na hivyo upungufu wa dunia hii haupo kabisa Peponi;**

Tutawaumba kwa umbo bora zaidi (56:35).

Umbile hili litakuwa na sifa zote bora zinazowafikiana na Pepo. Pale tunapolitafakari umbile linalowafikiana na sifa za Peponi, vigezo hivi vya uzuri wa wanawake hawa vinakuja fikirani; nywele zao zitakuwa safi na laini muda wote, ngozi yao itakuwa nyororo na ng'avu na harufu nzuri itakuwa ikitoka

kwenye viwiliwili vyao (Allahu A'alam). Sifa nyingine ya wanawake watakaozwa waumini Peponi ni kwamba wanarika (hirimu) moja;

Na pamoja nao watakuwepo wake zao watulizao macho kwa waume zao, hirimu zao (umri mmoja na wao). (38:52).

Wanasemwa kuwa wana macho haya;

Na pamoja nao watakuwa wanawake wenye macho mazuri makubwa (37:48).

Kuhusiana na hili aya nyingine inasema hivi;

Watakuwamo humo wanawake watulizao macho yao; Hajawagusa Binadamu wala Jini yejote kabla ya (waume zao) (55:56).

Wanawake hawa wanatajwa kama mayai yaliyohifadhiwa;

Wanawake hao kama mayai yaliyohifadhiwa (37:49).

Na kuhusu macho yao Qur'an inasema:

Na wanawake wenye macho mazuri na makubwa kama kwamba ni Lulu zilizofichwa (56:22-23).

Aya hizi zinatuthibitishia ukweli na imani kuwa wanawake hawa wameumbwa na wamehifadhiwa sehemu maalum kwa ajili ya waume zao tu. Neno kufichikana linaashiria kuwa ni vigumu kuwapata kwani thamani yao ni kubwa. Kule kufananishwa kwao na yai au lulu kuna maana kuwa haiba yao ni nzuri mno mwenye kuijuwa ni Mwenyewe Muumba aliyeaumba na

kuwapandikizia madaha na mbwembwe za umbile la kiwanauke kwa wanawake hao wa Peponi. Hamu na raha anayokuwa nayo mwanaume kwa mwanamke anayempenda aliye wake peke yake, kadhalika kwa mwanamke kwa mwanamme anayempenda na wanaooneshana ukarimu, huruma, mahaba na mapenzi ya kila namna huipa nafsi ya kila mmoja raha isiyoelezeka. Bila shaka chanzo cha hisia hizi kali lazima iumbwe katika nafsi ya Muumini kulingana na sifa za Peponi. Katika suratil Rahmani aya ya 70 Allah amewaelezea wanawake maalumu wa Peponi kuwa ni wazuri wa tabiya, warembo na wazuri wa sura:

Wamo humo wanawake wazuri (wa tabia), wazuri (wa sura na miili) (55:70).

Katika sura hiyo hiyo inabainishwa kuwa wake hawa wa waumini wapo kwa ajili ya waume zao tu. Neno hawajaguswa na mtu au Jini linashadidia ubikira wao. Suratil Wakiya aya ya 36 inatilia mkazo jambo hili kwa kusema kuwa tumewafanya kuwa waliotakasika. Sura ya 55:72 inasema wana macho meupe mazuri makubwa wanaotawishwa majumbani. Allah anawazungumzia hivi waumini na wake zao Peponi;

“Kwa yakini watu wa peponi leo wamo katika shughuli zao wamefurahi, wao na wake zao wamo katika vivuli wameegemea juu ya viti vyta fahari (36:55-56).

Pepo nje ya dhana

Mwenyezi Mungu anaelezea jozi ya waumini waume na wake zao Peponi kama ifuatavyo:

“Kwa yakini watu wa peponi leo wamo katika shughuli zao, wakiwa wamefurahi ; wao na wake zao wamo katika vivuli wameegemea katika viti vyta fahari”. (36:55-56).

Huko waumini wote wana wake zao wenyewe ambao wameumbwa vizuri wakiwa na sifa zote za uanauke na uzuri. Ni Wacha Mungu na wenye rika moja na waume zao:

“Tutawaumba kwa umbo (bora zaidi). Na tutawafanya vijana kama kwamba ndio kwanza wanaolewa. Wanapendana na waume zao walio hirimu moja na wao”.(56:35-37)

Hii inatupa elimu ya kuwa, hapa Duniani waume na wake walio waumini wanatakiwa kujengeana huba na mapenzi siyo kwa sababu ya maslahi ya kidunia bali kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (S.W). Katika suratil Ar-Rahmani aya ya 70 Allah anasema ; “Wamo humo wanawake wazuri (wa tabia) na wazuri wa sura pia”. Aya hii inabainisha kuwa wanawake hao wana haiba ya kupendeza, hawajaguswa kimaumbile na ni wasafi wa nafsi zao, wenye bashasha, wakarimu na wenye kila aina ya mvuto. Hapa yaweza kusemwa kuwa wana zile sura zenyewe hasa, zisizo na kasoro yoyote, ni wazuri wa sura na tabia. Katika suratil At-tur, aya ya 20, Mwenyezi Mungu anasema ; “Watakuwa wameegemea juu ya viti vya fahari vilivyopangwa safu safu, na Tutawaoza wanawake wanaopendeza wenye macho ya vikombe”.

Kwa kweli kufanya maongezi huku mkiwa mmekaa kwenye viti vya fahari kwa kuelekeana kuna raha ya aina yake. Pale tunapozungumza na mtu kwa kawaida huwa tunamtazama usoni mwake. Kwa hiyo kufanya maongezi mazuri na wanaume au wanawake wenye sura nzuri, wanaozungumza maneno ya kufurahisha katika makazi mazuri ambako Allah (S.W) anashukuriwa na kuhimidiwa, kutampa mtu starehe isiyoelezeka. Bila shaka, sifa za wanawake hawa haziishii usoni mwao tu, kwani kuanziya kichwani hadi vidoleni wameumbwa kwa urembo mkubwa. Surati Sad, aya ya 52 inasema ;

“Na pamoja nao watakuwemo wake zao watulizao macho kwa waume zao hirimu zao”.

Qur'an inawafananisha wanawake hao na Yakuti na Marijani madini ya thamani ambayo yanapendeza mno machoni ;

“Kama kwamba wao (wanawake hao) ni Yakuti na Marijani “.(55:58).

Kwa kuwafananisha na madini haya, Qur'an inashadidiya uzuri wa wanawake hao, hapa inajenga taswira kwa kuwafananisha na Yakuti na Marijani, maana yake ni kuelezeya jinsi walivyo warembo, rangi yao nzuri inayomeremeta. Kwa mlingano huu tu na kwa maelezo mengi mengineyo, waumini wanaweza kuelewa jinsi malipo aliyowaandalia Mwenyezi Mungu yalivyo makubwa kwa hiyo basi watu wwajipinde kutafuta radhi za Allah (S.W) na waombe rehema zake ili waingizwe peponi. Katika Qur 'an Mwenyezi Mungu ameziweka bayana neema za peponi kwani zipo nje ya uwezo wa kufikiri na hata kudhani. Peponi Allah (S.W) anawaruzuku waumini neema zisizo na hesabu ambazo jicho halijazona wala sikio halijasikiya.

“Watakuwa wanapitishiwa sahani za dhahabu na vikombe (vya dhahabu) : na vitakuwamo ambavyo nafsi inavipenda na macho yanavifurahia, na ninyi mtakaa humo milele”. (43:71).

Tunaweza kupata picha ya jumla ya jinsi Pepo ilivyo kutokana na fununu kuwa neema za pepo zinafanana na zile za Dunia hii, ingawa vifananavyo huweza kutafatautiana pakubwa,

“Na wabashirie walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwamba watapata mabustani yapitayo mito mbele yake; kila mara watakapopewa

matunda humo kuwa ni chakula watasema; haya ndiyo yale tuliyopewa zamani (ulimwenguni). Kwani wataletewa (matunda hayo) hali ya kuwa yamefanana na (yale waliyokuwa wakiyajua ulimwenguni . wataletewa kwa sura hiyo lakini utamu mwingine kabisa): na humo watapata wake walioutasika na watacaa milele”.(2: 25).

Kwa hayo maelezo na mifano iliyomo katika Qur'an, tunapata ufahamu fulani wakati tungali tukiishi katika dunia hii. Hata hivyo Mwenyezi Mungu katupa ufahamu huu kwa ajili tu ya kutupa picha Pepo ikoje lakini kwa kweli starehe na neema zake ziko nje kabisa ya ufahamu wetu. Kwa mfano ndani ya Pepo mna mito ya maji yasiyotibuka na mito ya maziwa ambayo ladha yake haibadiliki kamwe na mito ya vinywaji na mito ya asali. Jiografia hiyo haipo kabisa katika maumbile ya ulimwengu huu, Suratil Muhammad, aya ya kumi na tano inabainisha kuwa pepo inakusanya yote yaliyo mazuri ambayo hayawezi kulinganishwa na ya dunia hii:

Mfano wa pepo walioahidiwa wacha Mungu ni huu, imo mito ya maji yasiyovunda, na mito ya maziwa yasiyoharibika ladha yake na mito ya mvinyo wenye ladha kwa wanywao na mito ya asali iliyoafishwa; tena humo watapata matunda ya kila namna , na samahani kutoka kwa Mola wao. Basi je hao watakuwa sawa na wale watakao kaa mtoni na kunyweshwa maji yachemkayo yatakayo kata chango zao.

Aidha Hadithi inabainisha uzuri huo wa Pepo usio fikirika, Allah (S.W) kasema :Nimewaandalia waja wangu wanichao vitu ambavyo havijaonwa na jicho wala kusikiwa na sikio wala hata kufikiriwa na mwanadamu (Muslim). Katika aya moja: Mwenyezi Mungu anasema waumini wataishi katika Pepo kama wageni wake rasmi na waalikwa waliokaribishwa:

“Lakini waliomcha Mola wao watapata Mabustani (pepo) yanayopita mito mbele yake. Watacaa humo milele. Ndio makaribisho yao yatokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na vilivyopo kwa Mwenyezi Mungu ni starehe nzuri kabisa kwa watu wema (kuliko starehe hizi wanazozipata wabaya duniani)”. (3:198).

Katika aya hii Allah anaieleza Pepo kama ni sehemu ya raha, furaha , uhondo na starehe kubwa. Pale Dunia itakapofika mwisho wake na tukifaulu mtihani na kuyapata makazi haya halisi, kwa kweli, tutakuwa tumepata neema kubwa kweli kweli.

Hitimisho

Pepo ni makazi halisi ya Wanadamu, ni maisha halisi na ni mahali ambapo hapatakuwa na udhaifu wa kibinaadamu. Mwenye kunadi atanadi, mtakuwa na ubukheri wa afya wa milele, katu hamtaugua, mtakuwa na uhai wa milele, katu hamtakufa, mtakuwa na ujana wa milele katu hamtazeeka, na raha ya milele, katu hamtakuwa katika hali ya kutotosheka(Muslim). Qur'an inawaahidi Waumini kufaidi kukubwa na malipo yasiyokoma, na starehe za milele za maisha ya Peponi.

Peponi ni mahali pema pa maisha ya milele ambapo Allah (S.W) amepaandaa kwa malipo ya waja walioamini kama tulivyoona katika sura mbali mbali za kitabu hiki. Qur'an inaielezea kwa ufupi Pepo kwa kuyataja majumba ambayo watu wataishi humo, chakula watakachokula na vinywaji watakavyokunywa, nguo watakazovaa na vitu vizuri vizuri vitakavyokutwa humo. Tofauti na wengi wanavyodhani kuwa peponi kuna maisha ya kiroho, kwa hakika uhai na maisha ya Peponi, baada ya maisha ya ufu ya barzakh, ni wa maisha kama haya ya dunia bali yenyewe ni ya kudumu ni bora na halisi zaidi kuliko haya ya Dunia ambayo ni mchezo na starehe ya muda mfupi idanganyayo. Akiwa Peponi Mwanaadamu ataishi akiwa na umbile lake kamili bali lililobora zaidi ya hili alilonalo sasa. Maisha hayo ni mazuri mno yasiyostahili kulinganishwa na haya ya duniani licha ya kuwepo mambo yanayoonekana hufanana. Kutokana na mambo hayo, pale waumini wanapoyafariki maisha haya ya dunia na kwenda Barzakh kabla ya Akhera huwa hawapati hofu wala ugeni, hiyo ni kusema watayazoea maisha hayo kwa kukaribishwa na malaika na wenyeji wao vijana "*Wildanu Mukhalladuuun*" na wanawari waliotakasika "*Hurun iin*", hivyo watayazowea kirahisi tu. Maisha yao mapya ya milele yatakuwa kama yale waliyoishi hapa bali ya furaha isiyo na huzuni na ya starehe zaidi, kwahala ambako uchafu na uovu wote hautakuweko kabisa.

Kwa maneno mengine, watakuwa na vyakula na vinywaji bora, nguo maridadi kabisa, majumba mazuri, wake na waume. Kama isemavyo Qur'an, wataingia Peponi pamoja na wanawake ambao Allah amewazawadia kama malipo yao na watakaribishwa kwa shangwe na shamra shamra.

Ingieni bustanini Peponi nyinyi na wake zenu; mtafurahishwa humo (43:70).